**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**
**UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**


**04** # HISABATI

**Muda: Saa 1: 30** **Mwaka: 2020.**

**Maelekezo**

1. Mtihani huu una jumla ya maswali **matano (5)**
2. Jibu maswali **yote**

Katika swali la 1 – 5, kokotoa swali ulilopewa na kisha andika jibu sahihi kwenye nafasi iliyotolewa.

| Na. | | Swali | Sehemu ya Kazi | Jibu |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | (a) | Andika namba 12, 659 kwa maneno. | | |
| | (b) | Andika elfu kumi na moja mia moja kumi na moja kwa numerali.. | | |
| | (c) | Andika sehemu tatu ya nne katika tarakimu | | |
| | (d) | Andika sehemu iliyotiwa kivuli katika umbo lifuatalo:  | | |
| | (e) | Musa ana miaka 40. Andika umri wa Musa kwa kutumia numerali za kirumi. | | |
| **2.** | (a) | Panga namba zifuatazo kwa mpangilio unaoanza na namba kubwa hadi ndogo Zaidi:<br>125, 78, 111, 89, 305, 32, 120. | | |
| | (b) | Andika nmaba inayokosekana katika mfululizo ufuatao:<br>36, 33, 30 _____, 24. | | |
| | (c) | Andika namba mbili zinazofuatana katika mpangilio ufuatao:<br>X, XV, XX, XXV, _____, _______ | | |
| | (d) | Miti minne inatofautiana urefu kwa mpangilio ufuatao: m 5, m 8, m 11, m 14. Je, urefu wa mti wa tano utakuwa kiasi gani iwapo unafuata mpangilo huu? | | |




Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

| Na. | | Swali | Sehemu ya Kazi | Jibu |
|---|---|---|---|---|
| | (e) | Agnes alihesabu namba kwa kupunguza kumi ili kupata namba inayofuata. Iwapo namba ya kwanza ilikuwa 80, tafuta namba ya sita. | | |
| **3.** | (a) | Zidisha:<br>282<br>x 17<br>___ | | |
| | (b) | Baba alimpa Juma sarafu 10 za shilingi mia tano kila moja. Je, Juma alipewa kiasi gani cha pesa? | | |
| | (c) | Toa;<br>sh. 2, 750 – sh. 120 = | | |
| | (d) | Janeti alinunua vitu vifuatavyo sokoni: Machungwa 6 kila mja sh. 200, daftari moja kw ash. 2,000 na kalamu 3 kila moja sh. 700. Je, jumla alilipa shilingi ngapi? | | |
| | (e) | Jumlisha;<br>Saa dakika<br>5 38<br>+ 3 45<br>__________ | | |
| **4.** | (a) | Umbo lenye pande nne zinazolingana urefu huitwa _____ | | |
| | (b) | Nusu lita 10 za maji ni sawa na lita ngapi za maji? | | |
| | (c) | Badili gramu 16,000 kuwa kilogramu. | | |




Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

<table>
<tr><th colspan="2">Na.</th><th>Swali</th><th>Sehemu ya Kazi</th><th>Jibu</th></tr>
<tr><td></td><td>(d)</td><td>Bustani ya shule ina urefu wa m 25. Je, urefu huo ni sawa na sentimeta ngapi?</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td>(e)</td><td>Shule ya msingi Chatanda iko umbali wa km 2 kutoka barabara kuu. Je, shule hiyo ipo umbali wa meta ngapi kutoka barabara kuu?</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td>5.</td><td>(a)</td><td>Anold alifanya jaribio la Hisabati katika siku tatu za wiki, yaani Jumatatu, Jumatano na Ijumaa. Alama alizopata zimeoneshwa kwenye grafu ya mhimili ufuatao:</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td></td><td>

Je ni siku gani alipata alama za juu Zaidi?</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td>(b)</td><td>Jedwali lifuatalo linaonesha idadi ya wanafunzi wa darasa la tatu waliofaulu mtihani wa mwezi katiika shule ya msingi Kazamwendo.
<table>
<tr><th>Mwezi</th><th>Idadi ya Wanafunzi</th></tr>
<tr><td>Februari</td><td>68</td></tr>
<tr><td>Machi</td><td>74</td></tr>
<tr><td>Aprili</td><td>52</td></tr>
<tr><td>Mei</td><td>69</td></tr>
</table>
Je, ni mwezi gani wanafunzi wengi Zaidi walifaulu mtihani wa mwezi?</td><td></td><td></td></tr>
</table>



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

<table>
<tr><th colspan="2">Na.</th><th>Swali</th><th>Sehemu ya Kazi</th><th>Jibu</th></tr>
<tr><td></td><td>(c)</td><td>Wastani wa mauzo ya kalamu katika duka la Kapeto kwa siku nne yameoneshwa katika jedwali lifuatalo:
<table>
<tr><th>Siku</th><th>Mauzo</th></tr>
<tr><td>Jumatatu</td><td>Sh. 22,000</td></tr>
<tr><td>Jumanne</td><td>Sh. 21,000</td></tr>
<tr><td>Jumatano</td><td>Sh. 23,000</td></tr>
<tr><td>Alhamisi</td><td>Sh. 20,000</td></tr>
</table>
Mauzo madogo kuliko yote yalikuwa ni shilingi ngapi?</td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td>(d)</td><td>Idadi ya vitabu vya kusoma vilivyotolewa na serikali kwa miaka minne katika shule moja ni kama ifuatavyo:
<table>
<tr><td>Mwaka</td><td>Idadi</td></tr>
<tr><td>2002</td><td>132</td></tr>
<tr><td>2003</td><td>135</td></tr>
<tr><td>2004</td><td>142</td></tr>
<tr><td>2005</td><td>124</td></tr>
</table></td><td></td><td></td></tr>
<tr><td></td><td>(e)</td><td>Tani za mpunga zilizovunwa kwenye shamba la mkulima ziliongezeka sawia kila mwaka kwa miaka minne mfululizo na tani hizo zilioneshwa kwenye grafu ya mhimili ufuatao:


Je, jumla ya tani ngapi zilivunwa kwa miaka yote minne?</td><td></td><td></td></tr>
</table>



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org